BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2012

# MAARIFA YA JAMII

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2012

# MAARIFA YA JAMII

Kimechapishwa na
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2013

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO

DIBAJI....................................................................................................................iv
1.0 UTANGULIZI....................................................................................................1
2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA........................................1
2.1 Sehemu A: Uraia.............................................................................................1
2.2 Sehemu B: Historia.......................................................................................12
2.3 Sehemu C: Jiografia......................................................................................24
3.0 HITIMISHO....................................................................................................36
4.0 MAPENDEKEZO.............................................................................................36

# DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa somo la Maarifa ya Jamii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna wanafunzi walivyojibu maswali ya mtihani huo. Majibu ya wanafunzi katika mtihani ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha mambo ambayo wanafunzi waliweza kujifunza kwa ufasaha na yale ambayo hawakuweza kujifunza kwa ufasaha katika kipindi cha miaka saba ya Elimu ya Msingi.

Katika taarifa hii, mambo mbalimbali ambayo yamechangia watahiniwa kushindwa kujibu maswali kwa usahihi yameainishwa. Uchambuzi unaonesha kuwa yafuatayo yamechangia kuwafanya wanafunzi kutoweza kujibu maswali ya mtihani kwa usahihi: kushindwa kutambua matakwa ya swali; kuwa na uelewa mdogo wa mada mbalimbali; kutokuwa na ufahamu kabisa wa baadhi ya mada; kushindwa kuoanisha mada husika na maisha yao ya kila siku; kutojibu kabisa baadhi ya maswali au kuchagua jibu zaidi ya moja kinyume na maelekezo katika mtihani. Uchambuzi wa kila swali umefanyika ambapo dosari mbalimbali zilizojitokeza wakati watahiniwa walipokuwa wanajibu maswali zimeainishwa kwa kuonesha idadi ya watahiniwa waliojibu maswali kwa usahihi, walioshindwa kuchagua jibu sahihi, walioacha kujibu swali na ambao waliandika jibu zaidi ya moja katika swali husika.

Baraza la Mitihani Tanzania lina imani kuwa mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa lengo la kupatia ufumbuzi dosari zilizoainishwa katika taarifa hii. Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa, endapo maoni yaliyotolewa yatafanyiwa kazi ipasavyo, ujuzi na maarifa watakayoyapata wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi vitaoongezeka na hatimaye kiwango cha ufaulu katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kitaongezeka pia.

Mwisho, Baraza la Mitihani linapenda kutoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani, Makatibu Muhtasi na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii. Baraza litashukuru kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu kwa ujumla ambayo yatasaidia katika kuboresha taarifa ya uchambuzi wa maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa siku zijazo.

**Dkt. Joyce L. Ndalichako**
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa somo la Maarifa ya Jamii ulifanyika tarehe 20 mwezi Septemba mwaka 2012. Jumla ya watahiniwa 894,893 walisajiliwa kufanya mtihani huo. Kati ya watahiniwa waliosajiliwa kufanya mtihani huo, watahiniwa 865,281(96.69%) ndio waliofanya mtihani wa Maarifa ya Jamii. Uchambuzi wa majibu ya mtihani wa somo la Maarifa ya Jamii unaonesha kuwa watahiniwa 247,448 (28.61%) ndio waliofaulu mtihani huo.

Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa somo la Maarifa ya Jamii kwa mwaka 2012 ulikuwa na jumla ya maswali 50 yaliyogawanywa katika sehemu kuu tatu: Sehemu A: Uraia, sehemu B: Historia na sehemu C:Jiografia. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote . Aidha, watahiniwa walielekezwa kuchagua jibu sahihi kisha kuweka kivuli katika herufi ya jibu hilo kwa kila swali katika karatasi ya kujibia. Majibu ya watahiniwa yamefanyiwa uchambuzi na sababu zilizowafanya kuchagua majibu hayo zimeainishwa.

Taarifa hii imegawanywa katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inajumuisha uchambuzi wa majibu ya somo la Uraia, sehemu ya pili inaainisha uchambuzi wa majibu ya mtihani kwa somo la Historia na sehemu ya tatu inawasilisha uchambuzi wa somo la Jiografia.

# 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA

## 2.1 Sehemu A: Uraia

**Swali la 1:** Mwakilishi wa wananchi katika vikao vya Wilaya vya Serikali za Mitaa ni

A. Mkuu wa Wilaya
B. Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji
C. Afisa Mtendaji Kata
D. Mwenyekiti wa Wilaya wa Chama Tawala
E. Diwani wa Kata.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 237,375 | 215,842 | 113,340 | 68,446 | 226,723 | 1,335 | 2,108 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 27.44 | 24.95 | 13.10 | 7.91 | 26.21 | 0.15 | 0.24 |

Swali la 1 lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua mwakilishi wa wananchi katika vikao vya Wilaya vya Serikali za Mitaa. Jumla ya watahiniwa 226, 723 sawa na asilimia 26.21 waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni E "Diwani wa Kata". Asilimia 27.44 walichagua A "Mkuu wa Wilaya" ambalo halikuwa jibu sahihi. Watahiniwa hao hawakutambua kuwa Mkuu wa Wilaya ni Mteule wa Rais na hivyo si mwakilishi wa wananchi kwenye vikao vya wilaya. Diwani wa kata ambaye huchaguliwa kutokana na kura za wananchi ndiye mwakilishi wao. Aidha, asilimia 24.95 ya watahiniwa walichagua B "Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji" ambalo halikuwa jibu sahihi. Kuwapo kwa asilimia 26.21 tu ya watahiniwa walioweza kujibu swali hilo kwa usahihi kunaonesha kuwa watahiniwa wengi hawana uelewa wa muundo wa serikali za Mitaa na wajibu wa viongozi mbalimbali katika ngazi ya Kata, Kijiji na Wilaya.

**Swali la 2:** Mojawapo ya majukumu ya Halmashauri ya Wilaya ni kutoa ruzuku kwa

A. Serikali za Kata
B. Serikali Kuu
C. Vyama vya siasa
D. Serikali za vijiji
E. Mashirika yasiyo ya kiserikali.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 214,200 | 187,881 | 139,338 | 247,109 | 72,310 | 2,397 | 1,934 |
| Asilimia ya watahiniwa | 24.76 | 21.72 | 16.11 | 28.56 | 8.36 | 0.28 | 0.22 |

Swali la 2 lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua majukumu ya Halmashauri za Wilaya hususan katika utoaji wa ruzuku. Jumla ya watahiniwa 214,200 sawa na asilimia 24.76 waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni A "Serikali za Kata". Watahiniwa 247,109 sawa na asilimia 28.56 walichagua D "Serikali za Vijiji" ambalo halikuwa jibu sahihi kwa kuwa halmashauri hutoa ruzuku kwenye kata ambako kuna wataalamu wa fani mbalimbali. Kwa upande mwingine, asilimia 21.72 walichagua B "Serikali Kuu" ikimaanisha kuwa Halmashauri za Wilaya hutoa ruzuku kwa Serikali Kuu. Watahiniwa hao wanaonesha kutokuwa na uelewa wa mfumo mzima wa utoaji wa ruzuku kwani ruzuku hutolewa na Serikali Kuu kwenda kwenye Halmashauri na siyo kinyume chake. Aidha, asilimia 16.11 ya watahiniwa walichagua C "Vyama vya Siasa" hali iliyoonesha kuwa hawakuwa na uelewa kuhusu utaratibu wa utoaji wa ruzuku.

**Swali la 3:** Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya au Manispaa huteuliwa na:

A. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
B. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
C. Baraza la Madiwani la Halmashauri au Manispaa husika
D. Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
E. Katibu Mkuu Kiongozi.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 271,732 | 133,744 | 292,781 | 99,063 | 61,809 | 3,733 | 2,307 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 31.41 | 15.46 | 33.84 | 11.45 | 7.14 | 0.43 | 0.27 |

Swali la 3 lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua mwenye mamlaka ya kuteua Wakurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya au Manispaa. Swali hili ni miongoni mwa maswali ambayo watahiniwa hawakufanya vizuri kwani ni asilimia 15.46 tu ndiyo walioweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni B "Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania". Watahiniwa 292,781 walichagua C "Baraza la madiwani la Halmashauri au Manispaa husika" ambalo sio jibu sahihi. Baraza la madiwani huchagua Mwenyekiti wa Halmashauri lakini halihusiki katika uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri. Kwa upande mwingine watahiniwa 271,732 sawa na asilimia 31.41 walichagua A "Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania" ambalo halikuwa jibu sahihi, kwani Rais huteua Wakurugenzi wa Jiji na siyo wa Halmashauri za Wilaya. Inawezekana jibu hilo liliwavutia watahiniwa wengi kwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hufanya uteuzi wa viongozi mbalimbali. Hivyo, watahiniwa ambao hawakuwa na uelewa kuhusu mamlaka ya uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri walichagua A ambalo halikuwa jibu sahihi.

**Swali la 4:** Katika Bendera ya Taifa rangi ya kijani kibichi inawakilisha

A. Madini
B. Maji
C. Uoto wa asili
D. Kilimo
E. Ardhi.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 76,004 | 48,723 | 589,197 | 111,042 | 35,822 | 2,082 | 2,299 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 8.78 | 5.63 | 68.10 | 12.83 | 4.14 | 0.24 | 0.27 |

Swali la 4 lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua maana ya rangi za Bendera ya Taifa. Hivyo, walitakiwa kuonesha rangi ya kijani kibichi inatumika kuwakilisha nini. Watahiniwa wengi (68.10%) waliweza kujibu swali hilo kwa usahihi na kuchagua jibu sahihi C "uoto wa asili". Asilimia 12.83 ya watahiniwa walichagua D "kilimo" ambalo halikuwa jibu sahihi. Inawezekana watahiniwa hao walivutiwa na jibu hilo kwa sababu kutokana na kilimo mimea yenye rangi ya kijani kibichi hujitokeza. Hata hivyo hawakuwa wamesoma kwa umakini matakwa ya swali kwani rangi ya kijani kibichi huwakilisha uoto wa asili na siyo kilimo. Kwa upande mwingine asilimia 8.78 ya watahiniwa walichagua A "madini" ambalo halikuwa jibu sahihi. Watahiniwa wengine walichagua B "Maji" (5.63%) na E "ardhi" (4.14%) jambo linaloonesha kuwa hawajui tafsiri ya rangi zinazotumika kwenye bendera ya Taifa.

**Swali la 5:** Ni wakati gani Bendera ya Taifa hupeperushwa nusu mlingoti?

A. Wakati wa ziara za viongozi wa mataifa mengine.
B. Rais anapotangaza hali ya hatari.
C. Linapotokea janga la kitaifa au tukio la huzuni.
D. Siku ya kumbukumbu ya Mashujaa wa taifa.
E. Rais anapokuwa nje ya nchi.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 100,502 | 129,462 | 314,032 | 189,056 | 125,297 | 4,245 | 2,575 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 11.62 | 14.96 | 36.30 | 21.85 | 14.48 | 0.49 | 0.30 |

Swali la 5 lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua wakati ambapo Bendera ya Taifa hupepea nusu mlingoti. Asilimia 36.30 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi C "Linapotokea janga la kitaifa au tukio la huzuni". Aidha, asilimia 21.85 walichagua D, "Siku ya kumbukumbu ya mashujaa wa Taifa" hali inayoonesha kuwa hawakuwa na uelewa unaotakiwa. Kwa upande mwingine asilimia 14.96 ya watahiniwa walichagua B "Rais anapotangaza hali ya hatari" na asilimia 14.48 walichagua E "Rais anapokuwa nje ya nchi". Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa mazingira ambapo Bendera ya

Taifa hupeperushwa nusu mlingoti na kwa mtazamo wao waliona hali hiyo hutokea “linapotokea tukio linalomhusu Rais”. Aidha, asilimia 11.62 ya watahiniwa walichagua A “Wakati wa ziara za viongozi wa mataifa mengine” hali iliyoonesha kuwa hawakuwa na uelewa wa jibu sahihi kwani wakati wa ziara za viongozi bendera hupepea kama kawaida sio nusu mlingoti.

**Swali la 6:** Uchaguzi wa Rais na Wabunge hapa Tanzania hufanyika kila baada ya

A. Miaka 10
B. Miaka 3
C. Miaka 4
D. Miaka 5
E. Miaka 6.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 122,424 | 44,351 | 35,275 | 632,263 | 26,395 | 2,039 | 2,422 |
| Asilimia ya watahiniwa | 14.15 | 5.13 | 4.08 | 73.08 | 3.05 | 0.24 | 0.28 |

Swali la 6 lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua muda ambapo uchaguzi wa Rais na Wabunge hufanyika. Swali hili lilijibiwa vizuri kwani watahiniwa 632,263 sawa na asilimia 73.08 waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni D “Kila baada ya “Miaka mitano”. Hata hivyo watahiniwa 122,424 walichagua A “Kila baada ya miaka kumi”, ambalo halikuwa jibu sahihi. Inawezekana watahiniwa hao walivutiwa na jibu hilo kutokana na Rais kuruhusiwa na katiba kutawala kwa vipindi viwili vya miaka mitano endapo atachaguliwa na hivyo kufanya jumla ya miaka kumi. Majibu mengine B, C na E hayakuwavutia watahiniwa kwani ni asilimia ndogo tu ndiyo waliochagua.

**Swali la 7:** Haki za binadamu zinapaswa kutolewa kwa watu wote bila kujali

A. Vyama vya siasa
B. Katiba ya nchi
C. Haki za makundi maalumu
D. Umri wa mtu
E. Rangi, dini, jinsi  na kabila.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 71,508 | 72,120 | 70,730 | 122,805 | 523,021 | 2,024 | 2,961 |
| Asilimia ya watahiniwa | 8.27 | 8.34 | 8.18 | 14.19 | 60.45 | 0.23 | 0.34 |

Swali la 7 lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua maswala ya haki za binadamu na walipaswa kuainisha namna zinavyopaswa kutolewa. Asilimia 60.45 ya watahiniwa waliweza kujibu swali hilo kwa usahihi kwa kuchagua E " rangi, dini, jinsi na kabila" ambalo ndilo jibu sahihi. Aidha, asilimia 14.19 ya watahiniwa walichagua D "umri wa mtu" ambalo halikuwa jibu sahihi. Uwepo wa asilimia 14.19 ya watahiniwa waliochagua jibu hilo unaonesha kuwa huenda imejengeka imani miongoni mwa jamii kuwa yapo baadhi ya makundi ya watu hayatendewi haki kutokana na sababu za kiumri. Asilimia karibia 25 ya watahiniwa waliobaki ambao hawakuchagua jibu sahihi walikuwa wamegawanyika katika vipotoshi vifuatavyo; A "Vyama vya Siasa" (8.27%), B "Katiba ya nchi" (8.34%) na C "Makundi maalumu" (8.18%).

**Swali la 8:** Kazi mojawapo ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni

A. Kupokea na kuhakiki taarifa ya rasilimali na madeni ya viongozi wa umma
B. Kusuluhisha migogoro baina ya viongozi wa umma
C. Kufanya utafiti na kuelimisha jamii kuhusu haki za binadamu na utawala bora
D. Kuchunguza tuhuma zozote dhidi ya Afisa wa serikali anayehusishwa na rushwa
E. Kuthibitisha uteuzi wa mawaziri.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 206,707 | 167,919 | 296,943 | 128,567 | 57,607 | 4,791 | 2,635 |
| Asilimia ya watahiniwa | 23.89 | 19.41 | 34.32 | 14.86 | 6.66 | 0.55 | 0.30 |

Swali la 8 lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua majukumu ya sekretarieti ya maadili ya viongozi wa umma. Asilimia 23.89 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi ambalo ni A "Kupokea na kuhakiki taarifa ya rasilimali

na madeni ya viongozi wa umma". Watahiniwa 296,943 (34.32%) walichagua C "Kufanya utafiti na kuelimisha jamii kuhusu haki za binadamu na utawala bora". Aidha, asilimia 19.41 ya watahiniwa walichagua B "Kusuluhisha migogoro baina ya viongozi wa umma" ambayo hayakuwa majibu sahihi.

Kuwepo kwa watahiniwa wengi ambao hawakuweza kuchagua jibu sahihi kunaonesha wazi kuwa mada kuhusu majukumu ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma haikufundishwa ipasavyo. Kwa upande mwingine asilimia 14.86 ya watahiniwa walichagua D "Kuchunguza tuhuma zozote dhidi ya afisa wa serekali anayehusishwa na rushwa" ambalo halikuwa jibu sahihi. Hali hii inaonesha kuwa watahiniwa walishindwa kupambanua majukumu ya taasisi mbali mbali za serikali. Jukumu la kuchunguza suala la rushwa ni la Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na sio jukumu la Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

**Swali la 9:** Ni chombo gani chenye jukumu la kulinda nchi yetu na mipaka yake?

A. Jeshi la Polisi Tanzania
B. Jeshi la Magereza
C. Jeshi la Kujenga Taifa
D. Jeshi la wananchi la Tanzania
E. Jeshi la Mgambo.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D*** | **E** | **Hawakujibu** | **Nyingine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 273,710 | 60,409 | 147,614 | 313,915 | 64,342 | 2,467 | 2,712 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 31.64 | 6.98 | 17.06 | 36.28 | 7.44 | 0.29 | 0.31 |

Swali la 9 liliwataka watahiniwa kubainisha chombo chenye jukumu la kulinda nchi yetu na mipaka yake miongoni mwa vyombo vya ulinzi na usalama walivyopewa. Asilimia 36.28 ya watahiniwa wote walichagua D "Jeshi la Wananchi la Tanzania" ambalo ni jibu sahihi. Watahiniwa 273,710 ambao ni sawa na (31.64%) ya watahiniwa wote walichagua A "Jeshi la Polisi Tanzania" jambo linaloashiria kuwa mada ya ulinzi na usalama haikueleweka ipasavyo na hivyo kuwafanya watahiniwa kushindwa kubainisha majukumu ya majeshi yetu ya ulinzi na usalama. Aidha, asilimia 17.06 ya watahiniwa walichagua C "Jeshi la Kujenga Taifa". Inawezekana kuwepo kwa neno taifa katika jibu hili kuliwavutia watahiniwa kufikiri kuwa jeshi hili ndilo lenye jukumu la kulinda mipaka ya nchi. Asilimia 15 ya watahiniwa wote walichagua majibu B na E ambayo hayakuwa sahihi.

**Swali la 10:** Lengo kuu la Polisi Jamii ni

A. Kufundisha raia kazi za Polisi
B. Kujenga mahusiano ya kirafiki baina ya Polisi na raia
C. Kuwezesha Maafisa wa Polisi kuishi na raia
D. Kuwafanya raia kuwa wakakamavu kama Polisi
E. Kuzuia matumizi ya dawa za kulevya katika jamii.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 75,121 | 255,763 | 62,181 | 103,612 | 362,042 | 3,196 | 3,254 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 8.68 | 29.56 | 7.19 | 11.98 | 41.85 | 0.37 | 0.38 |

Swali la 10 lilikuwa linapima uelewa wa watahiniwa katika kutambua lengo la Polisi Jamii. Licha ya kuwa dhana hii imekuwa ikitangazwa kwenye vyombo vya habari na kupitia vipeperushi mbali mbali ni asilimia 29.56 tu ya watahiniwa ndio walioweza kupata jibu sahihi ambalo ni B "Kujenga mahusiano ya kirafiki baina ya polisi na raia." Asilimia 41.85 ya watahiniwa walichagua E "Kuzuia matumizi ya dawa za kulevya katika jamii" ambalo halikuwa jibu sahihi. Kuwepo kwa asilimia 41 ya watahiniwa ambao walionesha kuwa lengo la kuwa na polisi Jamii ni kuzuia matumizi ya dawa za kulevya kunaonesha kuwa watahiniwa wengi hawakuwa na uelewa wa dhana ya polisi jamii. Aidha, huenda jibu hilo lisilo sahihi limechaguliwa na watahiniwa wengi zaidi kuliko chaguzi nyingine zote kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa jamii. Kwa upande mwingine, asilimia 11.98 ya watahiniwa walichagua D "Kuwafanya raia kuwa wakakamavu kama polisi" jambo linaloonesha kuwa hawakuwa na uelewa kuhusu lengo la Polisi Jamii.

**Swali la 11:** Mila zinazoathiri afya ya uzazi wa kinamama ni pamoja na

A. Mahari na uzazi wa mpango
B. Ukeketaji wanawake na uzazi wa mpango
C. Ndoa za utotoni na mahari
D. Ukeketaji wanawake na ndoa za utotoni
E. Kunyonyesha watoto kwa muda mrefu.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 87,459 | 145,634 | 78,571 | 473,903 | 74,294 | 2,679 | 2,629 |
| Asilimia ya watahiniwa | 10.11 | 16.83 | 9.08 | 54.78 | 8.59 | 0.31 | 0.30 |

Swali la 11 liliwataka watahiniwa kutambua mila zinazoathiri afya ya uzazi wa kina mama miongoni mwa chaguzi walizopewa. Asilimia 54.78 ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni D "Ukeketaji wa wanawake na ndoa za utotoni." Aidha, asilimia 16.83 walichagua B "Ukeketaji wa wanawake na uzazi wa mpango" ambalo halikuwa jibu sahihi kwa kuwa uzazi wa mpango unaimarisha afya ya uzazi. Watahiniwa waliochagua jibu hilo hawakuwa makini katika kusoma swali na jibu kwa ukamilifu. Inawezekana kuwa walisoma sehemu ya kwanza inayohusu ukeketaji wa wanawake bila kuzingatia sehemu ya pili iliyohusu uzazi wa mpango. Aidha, kwa upande mwingine asilimia 10.11 ya watahiniwa walichagua A "Mahari na uzazi wa mpango" licha ya kwamba suala la mahari halina uhusiano kabisa na afya ya uzazi kwa kinamama. Inaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa kabisa wa mila zinazoathiri afya ya uzazi kwasababu uwepo wa neno mahari ulipaswa kuwafanya waone kuwa chaguzi A haikupaswa kuwa jibu sahihi. Watahiniwa waliochagua D "Ndoa za utotoni na mahari" walikuwa na tatizo la aina hiyo pia.

**Swali la 12:** Mojawapo ya changamoto wanazozipata wajasiriamali ni pamoja na

A. Ukosefu wa leseni za biashara
B. Kutokuwepo kwa benki na taasisi za fedha
C. Upatikanaji wa masoko ya bidhaa na huduma
D. Uwepo wa askari polisi na mgambo wengi maeneo ya mijini
E. Kutokuwepo sera ya uwekezaji.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 231,510 | 115,335 | 252,854 | 105,094 | 153,463 | 4,120 | 2,793 |
| Asilimia ya watahiniwa | 26.76 | 13.33 | 29.23 | 12.15 | 17.74 | 0.48 | 0.32 |

Swali la 12 liliwataka watahiniwa kubainisha miongoni mwa chaguzi walizopewa changamoto zinazowapata wajasiriamali. Asilimia 29.23 ya

watahiniwa walichagua jibu sahihi ambalo ni C “Upatikanaji wa masoko ya bidhaa na huduma”. Asilimia 26.76 ya watahiniwa walichagua A “Ukosefu wa leseni za biashara” ambalo halikuwa jibu sahihi kwa sababu mtu yeyote anayetaka kuwa mjasiriamali akifuata sheria na taratibu zilizowekwa na serikali anaweza kupata leseni bila usumbufu wowote.

Asilimia 17.74 ya watahiniwa walichagua E “Kutokuwepo sera ya uwekezaji” ambalo halikuwa sahihi kwani sera ya uwekezaji na uwezeshaji ipo tangu mwaka 1997. Asilimia 12.15 ya watahiniwa walichagua D “Uwepo wa askari polisi na mgambo wengi maeneo ya mijini”. Yawezekana watahiniwa hao walihusisha uwepo wa askari ambao hupambana na watu wanaovunja sheria kwa kufanya biashara maeneo yasiyoruhusiwa kuwa ni changamoto zinazowakabili wajasiriamali jibu ambalo sio sahihi. Asilimia 13.33 ya watahiniwa walichagua herufi B “Kutokuwepo kwa benki na taasisi za fedha” jambo ambalo sio sahihi kwani taasisi hizi zipo hadi katika ngazi ya wilaya na katika baadhi ya vijiji.

**Swali la 13:** Ni chombo gani chenye jukumu la kumchagua Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa?

A. Baraza la Udhamini la Umoja wa Mataifa.
B. Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa.
C. Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.
D. Sekretarieti ya Umoja wa Mataifa.
E. Mahakama Kuu ya Kimataifa.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 95,564 | 428,282 | 126,566 | 86,600 | 121,491 | 3,797 | 2,869 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 11.05 | 49.50 | 14.63 | 10.01 | 14.04 | 0.44 | 0.33 |

Swali la 13 lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua chombo chenye jukumu la kumchagua Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Asilimia 49.50 ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni B “Baraza kuu la Umoja wa Mataifa”. Watahiniwa waliobaki ambao ni kati ya asilimia 10.01 – 14.63 hawakuchagua jibu sahihi na waligawanyika katika chaguzi A, C, D na E. Kuwapo kwa idadi kubwa ya watahiniwa (49.50%) walioweza kutambua chombo kinachomchagua Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ikilinganishwa na asilimia 15.46 ya watahiniwa walioweza kutambua mamlaka ya uteuzi wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya katika swali la 3 kunaonesha kuwa wanafunzi wana uelewa zaidi kuhusu Umoja wa

Mataifa kuliko wanavyozielewa Halmashauri za Miji/Wilaya.

**Swali la 14:** Mtumishi wa umma ambaye ni Mbunge kwa mujibu wa nafasi yake katika utumishi wa umma ni

A. Jaji Mkuu
B. Katibu Mkuu Kiongozi
C. Mthibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
D. Msajili wa vyama vya siasa
E. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 274,158 | 137,292 | 182,339 | 77,402 | 186,392 | 4,592 | 2,994 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 31.69 | 15.87 | 21.08 | 8.95 | 21.54 | 0.53 | 0.35 |

Swali la 14 liliwataka watahiniwa kubainisha mtumishi wa umma ambaye ni Mbunge kwa mujibu wa nafasi yake katika utumishi wa umma. Swali hili ni miongoni mwa maswali ambayo hayakujibiwa vizuri kwani ni asilimia 21.54 tu ya watahiniwa ndio waliochagua jibu sahihi ambalo ni E “Mwanasheria Mkuu wa Serikali”. Asilimia 31.69 ya watahiniwa walichagua A “Jaji Mkuu” ambalo halikuwa jibu sahihi. Kuwepo kwa watahiniwa wengi zaidi waliochagua jibu hilo ikilinganishwa na waliochagua jibu sahihi kunaonesha kuwa huenda watahiniwa walishindwa kutofautisha kati ya Jaji Mkuu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, asilimia 21.08 ya watahiniwa walichagua C “Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali” na asilimia 15.87 ya watahiniwa walichagua B “Katibu Mkuu Kiongozi”. Hii inaonesha kuwa hawakuwa na uelewa kabisa wa matakwa ya swali.

Kimsingi swali hili lilipaswa kufanyika vizuri zaidi ukizingatia kuwa vipindi vya Bunge hurushwa moja kwa moja kweye vyombo vya habari. Hivyo, watahiniwa wangekuwa wanafuatilia kwa umakini wangeweza kutambua kwa urahisi kuwa ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiye anayeingia bungeni na sio Jaji Mkuu au viongozi wengine waliotajwa kwenye vipotoshi walivyopewa.

## 2.2 Sehemu B: Historia

**Swali la 15:** Mabaki ya Zinjanthropus yaligunduliwa

A. Kondoa
B. Kalenga
C. Olduvai
D. Isimila
E. Engaruka.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 186,393 | 67,743 | 426,525 | 99,921 | 78,496 | 3,554 | 2,537 |
| Asilimia ya watahiniwa | 21.54 | 7.83 | 49.30 | 7.83 | 9.07 | 0.41 | 0.29 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua mahali yalipogunduliwa mabaki ya Zinjanthropus. Asilimia 49.30 ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni C "Olduvai". Aidha, watahiniwa waliochagua A (21.54%), B (7.83%), D (7.83%) na E (9.07%) walishindwa kubainisha eneo yalipopatikana mabaki ya watu wa kale (Zinjanthropus) kati ya maeneo ya kihistoria yaliyokuwa yametajwa.

**Swali 16:** Wafanyabiashara wa mwanzo wa kigeni kuja Tanganyika walitoka

A. Amerika
B. Amerika kaskazini
C. Asia
D. Ulaya
E. Amerika kusini.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 53,573 | 85,018 | 338,473 | 285,385 | 96,854 | 3,314 | 2,552 |
| Asilimia ya watahiniwa | 6.19 | 9.83 | 39.12 | 32.99 | 11.19 | 0.38 | 0.29 |

Swali hili lilihitaji watahiniwa kujua sehemu walipotoka wafanyabiashara wa kigeni wa mwanzo kuja Tanganyika. Watahiniwa 338,473 (39.12%) walipata jibu sahihi ambalo ni C "Asia". Aidha, asilimia 32.99 ya watahiniwa waliochagua D "Ulaya" walishindwa kuelewa dhana ya wafanyabiashara wa "mwanzo" kwani wafanyabiashara kutoka Ulaya walikuja Tanganyika

kuanzia karne ya 15 wakitanguliwa na wafanyabiashara kutoka Bara la Asia ambao biashara yao na Afrika Mashariki ilishamiri katika karne ya 8. Watahiniwa waliochagua A "Amerika", B "Amerika Kaskazini" na E "Amerika kusini" ambao ni asilimia 27.21 walishindwa kuelewa kuwa hakuna biashara iliyoshamiri baina ya sehemu hizo na Tanganyika.

**Swali la 17:** Mojawapo ya athari ya utawala wa Waingereza katika visiwa vya Unguja ilikuwa

A. Kukomesha biashara ya utumwa
B. Kuanzishwa kwa dini ya kikristu
C. Kuondoa umaskini
D. Kuanzisha kilimo cha karafuu
E. Kuanzisha vyama vya siasa.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A*** | **B** | **C** | **D** | **E** | **Hawakujibu** | **Nyingine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 297,103 | 180,217 | 72,231 | 193,075 | 114,951 | 5,157 | 2,435 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 34.34 | 20.83 | 8.35 | 22.32 | 13.29 | 0.60 | 0.28 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua athari za utawala wa Waingereza katika visiwa vya Unguja. Watahiniwa 297,103 (34.34%) waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni A "Kukomesha biashara ya utumwa". Watahiniwa hawa waliweza kufahamu mchango mkubwa wa Waingereza katika kukomesha biashara hiyo kupitia mikataba ya mwaka 1822, 1845 na 1873. Aidha asilimia 20.83 waliochagua B "Kuanzishwa kwa dini ya kikristu" walishindwa kuelewa kuwa Ukristu ulienezwa katika Pwani ya Afrika Mashariki na Wareno waliofika katika karne ya 15. Asilimia 8.35 waliochagua C "Kuondoa umaskini" walishindwa kuelewa kuwa dhamira ya ukoloni ilikuwa ni unyonyaji na siyo kuondoa umaskini, asilimia 22.32 ya walichagua D "Kuanzisha kilimo cha karafuu" walishindwa kuelewa kuwa zao la karafuu lililetwa na Waarabu na siyo Waingereza na asilimia 13.29 ya waliochagua E "Kuanzisha vyama vya siasa" walishindwa kuelewa kuwa vyama vya siasa vilianzishwa na wazalendo ili kupinga ukoloni.

**Swali la 18:** Uchaguzi mkuu wa kwanza wa vyama vingi vya siasa katika Tanzania ulifanyika mwaka

A. 1992
B. 1990
C. 1961
D. 2005
E. 1995.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 273,038 | 86,064 | 179,631 | 93,475 | 228,940 | 1,748 | 2,273 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 31.56 | 9.95 | 20.76 | 10.80 | 26.46 | 0.20 | 0.26 |

Swali lilipima uwezo wa watahiniwa kujua lini uchaguzi mkuu wa kwanza wa vyama vingi vya siasa katika Tanzania ulifanyika. Licha ya ukweli kwamba, chaguzi mbalimbali hapa nchini zimekuwa zinatangazwa kwenye vyombo vya habari, ni asilimia 26.46 tu ya watahiniwa waliopata swali hili kwa kuandika jibu sahihi E "1995". Asilimia 31.56 ya watahiniwa waliochagua A "1992" walishindwa kutofautisha kati ya mwaka wa kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa na mwaka ambao uchaguzi mkuu wa vyama vingi ulifanyika. Watahiniwa 86,064 (9.95%) waliochagua B "1990" walishindwa kuelewa kuwa mwaka huo kulikuwa na uchaguzi wa mwisho wa chama kimoja na siyo wa vyama vingi. Aidha, asilimia 20.76 waliochagua C "1961" walishindwa kutofautisha kati ya mwaka ambao Tanganyika ilipata uhuru na mwaka wa uchaguzi wa vyama vingi na watahiniwa asilimia 10.80 waliochagua D "2005" walihusisha uchaguzi mkuu wa tatu wa vyama vingi kinyume na matakwa ya swali.

**Swali la 19:** Elimu kwa wote (UPE) nchini Tanzania ilianzishwa mwaka

A. 1974
B. 1970
C. 1972
D. 1980
E. 1977.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 142,572 | 182,472 | 211,063 | 174,694 | 147,708 | 4,063 | 2,597 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 16.48 | 21.09 | 24.40 | 20.19 | 17.07 | 0.47 | 0.30 |

Swali lilipima uwezo wa watahiniwa kujua lini Elimu kwa Wote (UPE) nchini Tanzania ilianzishwa. Asilimia 16.48 walipata jibu sahihi kwa kuandika A "1974". Hata hivyo, watahiniwa waliochagua vipotoshi B (21.09%) , C (24.40%), D (20.19%) na E (17.07%) hawakuwa na uelewa wa mwaka ambao mpango wa Elimu kwa Wote (UPE) ulianzishwa.

**Swali la 20:** Nchi ya Afrika iliyokuwa inafuata mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1980 ni

A. Zimbabwe
B. Tanzania
C. Botswana
D. Ghana
E. Ethiopia

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 212,239 | 227,762 | 133,922 | 162,420 | 121,755 | 3,985 | 3,086 |
| Asilimia ya watahiniwa | 24.53 | 26.33 | 15.48 | 18.77 | 14.07 | 0.46 | 0.36 |

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha nchi ya Afrika iliyokuwa inafuata mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1980. Ni watahiniwa wachache tu (15.48%) waliopata swali hili kwa kuandika C "Botswana" ambayo ni nchi pekee iliyokuwa inafuata mfumo wa vyama vingi katika kipindi hicho kwani nchi nyingine zilizotajwa katika vipotoshi vya swali hili baada ya kupata uhuru ziliamua kufuata mfumo wa chama kimoja cha siasa hivyo kufanya jumla ya watahiniwa 724,176 sawa na asilimia 83.7 waliochagua kati ya herufi A,B,D na E kukosa swali hili. Aidha, mfumo wa vyama vingi vya siasa ulianzishwa tena katika bara la Afrika baada ya mageuzi ya kisiasa na kiuchumi mwanzoni mwa miaka ya 1990.

**Swali la 21:** Makabila maarufu katika Afrika ya Mashariki yaliyojihusisha na biashara kabla ya ukoloni ni

A. Wangoni, Wakikuyu na Wachaga
B. Wayao, Wangoni na Wakikuyu
C. Wanyamwezi, Wayao na Wakikuyu
D. Wanyamwezi, Wayao na Wazaramo
E. Wayao, Wanyamwezi na Wakamba.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 132,642 | 132,421 | 211,801 | 172,943 | 207,855 | 4,454 | 3,053 |
| Asilimia ya watahiniwa | 15.33 | 15.31 | 24.48 | 19.99 | 24.02 | 0.51 | 0.35 |

Swali lilitahini uwezo wa watahiniwa kubaini makabila maarufu katika Afrika ya Mashariki yaliyojihusisha na biashara kabla ya ukoloni. Ni asilimia 24.02 tu ya watahiniwa walioweza kupata jibu sahihi ambalo ni E “Wayao, Wanyamwezi na Wakamba”. Watahiniwa hawa waliweza kutambua mchango wa makabila haya katika kuongoza misafara ya biashara ya Kaskazini (Wakamba) Kati (Wanyamwezi) na Kusini (Wayao). Aidha, asilimia 75.11 ya watahiniwa waliochagua vipotoshi vingine walishindwa kuzingatia maneno “makabila maarufu” yaliyokuwa kwenye kiini cha swali hivyo kuchagua makabila ambayo hayakuwa maarufu kwa kazi hiyo.

**Swali la 22:** Familia inaweza kujikwamua kiuchumi iwapo

A. Mama atajishughulisha na kazi za ndani
B. Baba ataajiriwa
C. Watoto watajishughulisha na masomo
D. Wanafamilia watatimiza wajibu wao
E. Wanafamilia watasali pamoja.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 75,624 | 105,471 | 210,793 | 422,183 | 45,345 | 3,046 | 2,707 |
| Asilimia ya watahiniwa | 8.74 | 12.19 | 24.36 | 48.80 | 5.24 | 0.35 | 0.31 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kubaini jinsi familia inavyoweza kujikwamua kiuchumi. Watahiniwa wengi walitarajiwa kupata swali hili kwani licha ya kuwa mada ya Elimu ya Familia inafundishwa darasani, suala la kujikwamua kiuchumi ni dhana inayotekelezwa kwa vitendo katika familia nyingi. Hata hivyo ni asilimia 48.80 tu ya watahiniwa waliochagua jibu sahihi ambalo ni D “Wanafamilia watatimiza wajibu wao”. Jibu hili lilikuwa lina hoja inayojumuisha wajibu wa wanafamilia wote kwa pamoja tofauti na vipotoshi vingine kwa mfano A “Mama atajishughulisha na kazi za ndani” (8.74%) , B “Baba ataajiriwa” (12.19%) na C “Watoto watajishughulisha na masomo” (24.36%) ambavyo havikujumuisha wanafamilia wote. Aidha, asilimia 5.24 waliochagua E “Wanafamilia watasali pamoja” walishindwa kuelewa kuwa kujikwamua kiuchumi hakuwezi kusababababishwa na kusali tu.

**Swali la 23:** Kabla ya ukoloni elimu ya jadi ilitolewa kwa njia ya

A. Sheria za serikali
B. Jando na unyago
C. Kwenda vitani
D. Kusoma vitabu
E. Shule za awali

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 116,975 | 393,461 | 102,008 | 90,945 | 155,258 | 3,251 | 3,271 |
| Asilimia ya watahiniwa | 13.52 | 45.48 | 11.79 | 10.51 | 17.95 | 0.38 | 0.38 |

Swali lililenga kupima uwezo wa watahiniwa kubaini njia iliyotumika kutoa elimu ya jadi kabla ya ukoloni. Watahiniwa wengi (45.48%) waliweza kuandika jibu sahihi ambalo ni B "Jando na unyago". Watahiniwa waliojibu D "Kusoma vitabu" (10.51%), na E "Shule za awali" (17.95%) walishindwa kuelewa kuwa elimu kupitia usomaji wa vitabu na shule za awali ilitolewa baada ya ukoloni. Aidha, asilimia 13.52 ya watahiniwa waliochagua A "Sheria za serikali" walishindwa kubaini kuwa kabla ya ukoloni hapakuwa na sheria za serikali na watahiniwa asilimia 11.79 waliojibu C "Kwenda vitani" walishindwa kuelewa kuwa siyo wanajamii wote waliokwenda vitani hivyo njia hii isingefaa kutoa elimu kwa wote.

**Swali la 24:** Makoloni ya Ujerumani katika Afrika yalikuwa

A. Naijeria, Namibia na Togo
B. Gambia, Togo na Namibia
C. Kameruni, Togo na Namibia
D. Namibia, Tanganyika na Naijeria
E. Kameruni, Tanganyika na Senegal.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 117,099 | 104,026 | 112,544 | 349,140 | 174,538 | 4,624 | 3,198 |
| Asilimia ya watahiniwa | 13.53 | 12.02 | 13.01 | 40.36 | 20.17 | 0.53 | 0.37 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kubainisha makoloni ya Ujerumani katika Afrika. Watahiniwa wengi (40.36%) walikosa swali hili kwa kuchagua D "Namibia, Tanganyika na Naijeria" ambalo halikuwa jibu sahihi

kwani Naijeria lilikuwa koloni la Uingereza hivyo pia kufanya asilimia 13.53 ya watahiniwa waliochagua kipotoshi A “Naijeria, Namibia na Togo” kukosa swali hili. Aidha, Makoloni kama Gambia na Senegal yaliyopo kwenye vipotoshi hayakuwa makoloni ya Ujerumani hivyo kufanya kipotoshi B “Gambia, Togo na Namibia” kilichojibiwa na asilimia 12.02 ya watahiniwa na E “Kameruni, Tanganyika na Senegal” kilichojibiwa na asilimia 20.17 ya watahiniwa kutokuwa sahihi. Ni watahiniwa asilimia 13.01 tu walioweza kupata swali hili kwa kuandika herufi ya jibu sahihi C “Kameruni, Togo na Namibia”.

**Swali la 25:** Ni mataifa yapi kati ya yafuatayo yalianzisha umoja wa nchi zisizofungamana na upande wowote?

A. Ulaya mashariki
B. Nchi zinazoendelea
C. Ulaya magharibi
D. Amerika ya kusini
E. Amerika ya kaskazini.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 118,056 | 250,583 | 139,223 | 212,814 | 136,540 | 4,974 | 2,979 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 13.65 | 28.96 | 16.09 | 24.60 | 15.78 | 0.57 | 0.34 |

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha mataifa yaliyoanzisha umoja wa nchi zisizofungamana na upande wowote. Asilimia 28.96 ya watahiniwa waliandika B “Nchi zinazoendelea” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya dhana ya kutofungamana na upande wowote hivyo kubaini jibu sahihi. Aidha, asilimia 13.65 ya watahiniwa waliojibu A “Ulaya Mashariki”, asilimia 16.09 ya watahiniwa waliojibu C “Ulaya Magharibi”, asilimia 24.60 ya watahiniwa waliojibu D “Amerika ya Kusini” na asilimia 15.78 ya watahiniwa waliochagua E “Amerika ya Kaskazini” walishindwa kuelewa dhana ya nchi zisizofungamana na upande wowote hivyo kuzihusisha nchi zilizoendelea.

**Swali la 26:** Wajerumani walitawala Tanganyika baada ya

A. Vita Kuu ya Kwanza
B. Vita Kuu ya Pili
C. Mkutano wa Berlin
D. Kuundwa kwa UNO
E. Kushindwa kwa Wareno.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 218,366 | 187,894 | 267,219 | 82,351 | 102,785 | 3,591 | 2,963 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 25.24 | 21.72 | 30.89 | 9.52 | 11.88 | 0.42 | 0.34 |

Swali lilitahini uelewa wa watahiniwa juu ya kipindi ambacho wajerumani waliitawala Tanganyika. Asilimia 30.89 ya watahiniwa walipata swali hili kwa kuandika C "Mkutano wa Berlin" kwani baada ya mkutano huo ndipo makoloni yaligawanywa na Tanganyika ikawa chini ya Ujerumani. Aidha watahiniwa wengi (25.24%) walichagua A "Vita Kuu ya Kwanza" ambalo halikuwa jibu sahihi kwani watahiniwa hawa walishindwa kuelewa kuwa baada ya vita kuu ya kwanza, Ujerumani ilinyang'anywa makoloni yake yote na Tanganyika ikawa chini ya Uingereza. Aidha, asilimia 21.72 walichagua B "Vita Kuu ya Pili" ambalo pia halikuwa jibu sahihi kwani kipindi hicho Ujerumani ilishanyang'anywa makoloni yake na ilianzisha vita hiyo ili kujaribu kuyakomboa. Watahiniwa waliochagua D "Kuundwa kwa UNO" (9.52%) na E "Kushindwa kwa Wareno" (11.88%) walishindwa kuelewa mtiririko wa matukio ya kihistoria kwani UNO iliundwa mara baada ya vita kuu ya pili ya dunia na Wareno waliondoka pwani ya Tanganyika hata kabla ya mgawanyo wa makoloni.

**Swali la 27:** Katika Zama za Mwanzo za Mawe binadamu

A. Alianza kufuga wanyama na ndege
B. Aligundua moto
C. Alijihusisha na kilimo na biashara
D. Aliongeza uwezo wa kuzalisha chakula
E. Aliishi kwa kutegemea mazingira.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 102,988 | 311,206 | 79,384 | 79,666 | 285,394 | 2,728 | 3,803 |
| Asilimia ya watahiniwa | 11.90 | 35.97 | 9.18 | 9.21 | 32.99 | 0.32 | 0.44 |

Swali hili lilitahini ufahamu wa watahiniwa juu ya maendeleo ya maisha ya binadamu wakati wa Zama za Mwanzo za Mawe. Watahiniwa wengi (35.97%) walichagua B "Aligundua moto" ambalo sio jibu sahihi kwani moto uligunduliwa wakati wa zama za kati. Aidha, asilimia 11.90 walichagua A "Alianza kufuga wanyama na ndege", asilimia 9.18 walichagua C "Alijihusisha na kilimo na biashara" na asilimia 9.21 walichagua D "Aliongeza uwezo wa kuzalisha chakula" ambayo pia hayakuwa majibu sahihi kwani yote yalitokea baada ya zama za mwanzo. Ni watahiniwa (32.99%) tu walioweza kutoa jibu sahihi E "Aliishi kwa kutegemea mazingira".

**Swali la 28:** Jamii zilizokuwa maarufu kwa kufua chuma hapa Tanganyika ni pamoja na

A. Wapare na Wazinza
B. Wapare na Wagogo
C. Wazinza na Wasukuma
D. Wapare na Wajaluo
E. Wazinza na Wagogo.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 168,373 | 230,518 | 188,098 | 162,455 | 107,486 | 5,153 | 3,086 |
| Asilimia ya watahiniwa | 19.46 | 26.64 | 21.74 | 18.78 | 12.42 | 0.60 | 0.36 |

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha jamii zilizokuwa maarufu katika ufuaji wa chuma hapa Tanganyika. Jumla ya watahiniwa 168,373 sawa na asilimia 19.46 walipata swali hili kwa kuchagua jibu sahihi A "Wapare na Wazinza". Aidha, jumla ya watahiniwa 688,557 sawa na asilimia 79.58 walikosa swali hili kwa kuchagua vipotoshi ambavyo vilikuwa na jamii ambazo siyo maarufu kwa ufuaji wa chuma bali zilikuwa maarufu kwa ufugaji mfano Wagogo na Wasukuma na utengenezaji wa vyungu mfano Wajaluo.

**Swali la 29:** Soko kuu la watumwa Zanzibar lilifungwa mwaka

A. 1873
B. 1822
C. 1845
D. 1820
E. 1900.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 304,284 | 146,914 | 230,860 | 77,827 | 97,325 | 4,642 | 3,317 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 35.17 | 16.98 | 26.68 | 9.00 | 11.25 | 0.54 | 0.38 |

Swali hili liliwataka watahiniwa kubainisha mwaka ambao soko kuu la utumwa Zanzibar lilifungwa. Asilimia 35.17 walipata swali hili kwa kuandika herufi ya jibu sahihi A “1873”. Aidha, asilimia 16.98 ya watahiniwa waliochagua B “1822” na asilimia 26.68 walichagua C “1845” walikosa swali hili kwani walihusisha miaka ambayo mikataba mbalimbali iliyolenga kukomesha biashara ya utumwa iliposainiwa kinyume na matakwa ya swali. Hata hivyo, asilimia 9.0 ya watahiniwa waliochagua D “1820” na asilimia 11.25 ya watahiniwa waliochagua E “1900” hawakuwa na uelewa wowote juu ya swali hili kwani miaka hiyo haina uhusiano wa moja kwa moja na ukomeshaji wa biashara ya utumwa.

**Swali la 30:** Mojawapo ya athari za kugawanywa kwa bara la Afrika ilikuwa

A. Kukua kwa viwanda vya Waafrika
B. Kudumaa kwa viwanda vya Afrika
C. Kuboreshwa kwa uchumi wa jadi
D. Kudumisha utamaduni wa Kiafrika
E. Kuanza kwa biashara ya utumwa.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 115,531 | 215,039 | 124,262 | 174,797 | 226,690 | 4,978 | 3,872 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 13.35 | 24.86 | 14.36 | 20.20 | 26.20 | 0.58 | 0.45 |

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha athari za kugawanywa kwa Bara la Afrika. Jumla ya watahiniwa 215,039 sawa na asilimia 24.86 walipata

swali hili kwa kuchagua jibu sahihi B “Kudumaa kwa viwanda vya Afrika”. Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya athari za ukoloni kwa viwanda vilivyokuwepo kabla ya uvamizi wa kikoloni. Asilimia 47.91 ya watahiniwa waliojibu A “Kukua kwa viwanda vya Waafrika”, C “Kuboreshwa kwa uchumi wa jadi” na D “Kudumisha utamaduni wa Kiafrika” walihusisha ukoloni na maendeleo ya viwanda, uchumi na utamaduni wa Afrika mambo ambayo siyo sahihi kwani wakoloni walikuwa na athari hasi katika sekta hizo. Aidha asilimia 26.20 ya watahiniwa waliojibu E “Kuanza kwa biashara ya utumwa” walihusisha kipindi cha ukoloni na biashara ya utumwa jambo ambalo siyo sahihi kwani utumwa ulikomeshwa kabla ya ukoloni.

**Swali la 31:** Taifa la pili kuitawala Zanzibar lilikuwa

A. Uingereza
B. Ujerumani
C. Ureno
D. Oman
E. Ufaransa.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A*** | **B** | **C** | **D** | **E** | **Hawakujibu** | **Nyingine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 292,891 | 249,737 | 130,983 | 95,830 | 88,238 | 4,092 | 3,398 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 33.85 | 28.87 | 15.14 | 11.08 | 10.20 | 0.47 | 0.39 |

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha taifa la pili kuitawala Zanzibar. Watahiniwa wengi (33.85%) walipata swali hili kwa kuandika A “Uingereza”. Aidha watahiniwa 249,737 sawa na asilimia 28.87 walikosa swali hili kwa kuandika B “Ujerumani”. Watahiniwa hawa walihusisha utawala wa Wajerumani katika Tanganyika lakini walishindwa kuelewa kuwa Zanzibar haikuwa imeungana na Tanganyika katika kipindi hicho. Asilimia 15.14 waliojibu C “Ureno” na asilimia 10.20 ya waliojibu E “Ufaransa” hawakuwa na uelewa wa swali hili kwani Wareno na Wafaransa hawakuitawala Zanzibar na watahiniwa 95,830 sawa na asilimia 11.08 waliochagua D “Oman” walishindwa kuelewa kuwa utawala wa Sultani kutoka Omani ulikuwa wa mwanzo.

**Swali la 32:** Bidhaa zilizoletwa Tanganyika kutoka Bara la Asia kuanzia karne ya nane zilikuwa ni pamoja na

A. Pembe za ndovu na dhahabu
B. Ngozi na bunduki
C. Chumvi na shaba
D. Nguo na ngano
E. Nguo na watumwa.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 410,175 | 111,970 | 129,919 | 154,906 | 51,052 | 3,933 | 3,214 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 47.41 | 12.94 | 15.02 | 17.90 | 5.90 | 0.45 | 0.37 |

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha bidhaa zilizoletwa Tanganyika kutoka Bara la Asia kuanzia karne ya nane. Jumla ya watahiniwa 154,906 sawa na asilimia 17.90 walipata swali hili kwa kuchagua jibu sahihi D “Nguo na ngano”. Aidha, watahiniwa wengi walikosa swali hili kwa kuchagua vipotoshi ambavyo havikuwa na bidhaa zilizoletwa mfano asilimia 47.41 ya watahiniwa walichagua A “Pembe za ndovu na dhahabu” ambazo ni bidhaa zilizochukuliwa kutoka Afrika na siyo kuletwa na wafanyabiashara hao na asilimia 12.94 ya watahiniwa walichagua B “Ngozi na bunduki” ambapo ngozi ni moja ya bidhaa zilichukuliwa na siyo kuletwa. Aidha, asilimia 15.02 ya watahiniwa waliochagua C “Chumvi na shaba” walishindwa kuelewa kuwa bidhaa hizi zilipatikana Afrika na wafanyabiashara wa kigeni walikuja kuzitafuta na asilimia 5.90 ya watahiniwa waliochagua E “Nguo na watumwa” hawakuelewa kuwa watumwa walikuwa ni bidhaa muhimu kutoka Afrika katika kipindi hicho.

## 2.3 Sehemu C: Jiografia

**Swali la 33:** Katika kuonesha mahali kwa kutumia mistari ya gridi katika ramani huanza kusomwa namba za mstari gani?

A. Ulalo halafu wima.
B. Wima halafu ulalo.
C. Kushoto halafu kulia.
D. Kulia halafu juu.
E. Kulia halafu kushoto.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 364,911 | 271,345 | 101,723 | 54,818 | 66,455 | 3,070 | 2,847 |
| Asilimia ya watahiniwa | 42.18 | 31.36 | 11.76 | 6.34 | 7.68 | 0.35 | 0.33 |

Swali hili lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu namna ya kusoma mistari ya gridi katika ramani. Asilimia 42.18 ya watahiniwa walishindwa kutambua namna sahihi ya kusoma mistari ya gridi kwa kuchagua A "Ulalo halafu wima" ambalo ni kinyume cha jibu sahihi. Ni asilimia 31.36 tu ya watahiniwa waliweza kutambua chaguo B "Wima halafu ulalo" kuwa ni jibu sahihi kwani katika usomaji wa mistari ya gridi mistari inayoongezeka ukubwa wa nyuzi kuelekea mashariki ambayo ni mistari ya wima husomwa kwanza na kufuatiwa na mistari ambayo inaongezeka ukubwa wa nyuzi kuelekea kaskazini ambayo ni mistari ya ulalo. Watahiniwa waliochagua C (11.76%), D (6.34%) na E (7.68%) hawakufahamu namna sahihi ya kusoma mistari ya gridi katika ramani. Aidha asilimia ndogo sana 0.35 ya watahiniwa hawakujibu swali hili.

**Swali la 34:** Mambo muhimu ya kuzingatia katika uendeshaji wa shughuli za uchukuzi ni

A. Mtaji, sura ya nchi, uzalishaji na biashara
B. Teknolojia, serikali, mtaji na biashara
C. Mtaji, sura ya nchi, watu na viwanda
D. Serikali, mashirika, mtaji na watu
E. Teknolojia, mtaji, uzalishaji na biashara.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 184,967 | 145,098 | 142,868 | 96,842 | 288,544 | 3,963 | 2,887 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 21.38 | 16.77 | 16.51 | 11.19 | 33.35 | 0.46 | 0.33 |

Swali hili lilitahini uelewa wa watahiniwa kuhusu mambo muhimu katika uendeshaji wa shughuli za uchukuzi. Idadi ya ufaulu wa watahiniwa ina mtawanyiko katika uchaguzi wa majibu yao ambapo ni asilimia 33.35 tu ya watahiniwa waliweza kujibu swali kwa usahihi kwa kuchagua E "Teknolojia, mtaji, uzalishaji na biashara". Aidha asilimia 21.38 ya watahiniwa waliandika chaguo A ambalo lina 'sura ya nchi' lakini halina 'teknolojia' ambayo ni muhimu katika uendeshaji wa shughuli za uchukuzi kwani ukiwa na teknolojia unaweza kuendesha shughuli za uchukuzi kwa urahisi zaidi. Asilimia 16.51 ya watahiniwa waliochagua C "Mtaji, sura ya nchi, watu na viwanda", walishindwa kutambua kuwa watu na viwanda si mahitaji muhimu katika uendeshaji wa shughuli za uchukuzi.

**Swali la 35:** Biashara ya ndani ni ile inayohusisha bidhaa

A. Zinazotengenezwa nje ya nchi
B. Zinazotengenezwa na kuuzwa ndani ya nchi
C. Zinazozalishwa ndani ya nchi
D. Zinazotengenezwa na kuuzwa nje ya nchi
E. Zinazouzwa nje ya nchi.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 104,839 | 423,663 | 200,827 | 87,474 | 44,451 | 1,757 | 2,158 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 12.12 | 48.97 | 23.21 | 10.11 | 5.14 | 0.20 | 0.25 |

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha bidhaa ambazo zinahusisha biashara ya ndani. Hili ni moja kati ya maswali ambayo yalikuwa na ufaulu mzuri kwani asilimia 48.97 ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni B "zinazotengenezwa na kuuzwa ndani ya nchi". Hii inaonesha kuwa watahiniwa hao wana ufahamu mkubwa kuhusu biashara ya ndani. Asilimia 23.21 ya watahiniwa walichagua C 'Zinazozalishwa ndani ya nchi' ambayo ni kweli inahusisha biashara ya ndani, lakini, watahiniwa hao hawakubaini kuwa ili iitwe biashara ya ndani bidhaa zinatakiwa pia kuuzwa

ndani ya nchi. Asilimia 27.37 ya watahiniwa walichagua kati ya chaguzi A "Zinazotengenezwa nje ya nchi", D "Zinazotengenezwa na kuuzwa nje ya nchi" na E "Zinazouzwa nje ya nchi" jambo linaloonesha kuwa hawafahamu biashara ya ndani inahusisha bidhaa za aina gani.

**Swali la 36:** Iwapo umbali wa kilometa 25 kwenye ardhi unawakilishwa na urefu wa sentimeta 5 kwenye ramani, kipimio cha ramani ni

A. 1:20000
B. 1:100000
C. 1:50000
D. 1:500000
E. 1:10000.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D*** | **E** | **Hawakujibu** | **Nyingine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 120,234 | 118,380 | 285,840 | 267,459 | 66,868 | 3,726 | 2,662 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 13.90 | 13.68 | 33.04 | 30.91 | 7.73 | 0.43 | 0.31 |

Swali lilimtaka mtahiniwa kukokotoa kipimio cha ramani, ikiwa amepewa urefu katika ardhi na urefu katika ramani. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa ni wa kuridhisha ukilinganishwa na ufaulu katika maswali mengine ya sehemu C kwani asilimia 30.91 ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi D "1:500000". Hii inaashiria kuwa watahiniwa hawa wanafahamu namna ya kukokotoa kipimio cha ramani kama ifuatavyo:

Njia:

Kipimio = $\dfrac{umbali\ katika\ ramani}{umbali\ katika\ ardhi}$

$= \dfrac{Sentimita\ 5}{Kilomita\ 25}$

Ikiwa km 1 = sm 100000

$= \dfrac{Sm\ 5}{Sm\ 2500000}$

Kipimio = 1: 500000

Asilimia 33.04 ya watahiniwa walichagua C "1:50000" ambapo walikokotoa

jibu kwa kutumia kanuni ya sentimita moja katika ardhi inawakilishwa na sentimita 10,000 katika ramani. Aidha, watahiniwa waliochagua A (13.90%), B (13.68%) na E (7.73%) walikuwa hawana uelewa wa namna ya kukokotoa kipimio cha ramani.

**Swali la 37:** Jua la utosi katika mwezi Disemba huwa katika

A. Kizio cha Kusini
B. Tropiki ya Kansa
C. Ikweta
D. Kizio cha Kaskazini
E. Tropiki ya Kaprikoni.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 91,636 | 253,707 | 237,207 | 88,607 | 186,231 | 4,596 | 3,185 |
| Asilimia ya watahiniwa | 10.59 | 29.32 | 27.42 | 10.24 | 21.53 | 0.53 | 0.37 |

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha sehemu ya dunia ambayo hupata jua la utosi katika mwezi Disemba. Watahiniwa wachache (21.53%) waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni E "Tropiki ya kaprikoni". Asilimia 29.32 ya watahiniwa walichagua B "Tropiki ya Kansa" ambayo hupata jua la utosi katika mwezi Juni. Watahiniwa waliochagua A (10.59%), C (27.42%) na D (10.24) hawakuwa na uelewa wa swali. Hata hivyo asilimia 0.53 ya watahiniwa hawakujibu swali hili.

**Swali la 38:** Bainisha vyanzo vya umeme kati ya vifuatavyo:

A. Nguvu ya maji, madini na nyaya
B. Upepo, nguvu ya maji na transfoma
C. Nguvu ya maji, upepo na jua
D. Makaa ya mawe, nyaya na transfoma
E. Nguvu ya maji, transfoma na makaa ya mawe.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 110,290 | 157,170 | 353,527 | 91,850 | 144,985 | 3,984 | 3,363 |
| Asilimia ya watahiniwa | 12.75 | 18.17 | 40.86 | 10.62 | 16.76 | 0.46 | 0.39 |

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha vyanzo vya umeme. Hili ni kati ya maswali ambayo yalikuwa na ufaulu mzuri kwani asilimia 40.86 ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni C “Nguvu ya maji, upepo na jua”. Watahiniwa wengine waliochagua A (12.75%), B (18.17%), D (10.62%) na E (16.76%) walishindwa kutofautisha vyanzo vya umeme na vifaa mbalimbali vinavyotumika katika ufuaji na usafirishaji wa umeme kama vile makaa ya mawe, madini, transfoma na  nyaya.

**Swali la 39:** Picha iliyopigwa katika uoto wa savana huonesha

A. Misitu minene
B. Nyasi ndefu
C. Miti iliyochongoka juu
D. Miti yenye umbile la mwamvuli
E. Nyasi fupi.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 289,524 | 177,017 | 90,467 | 157,766 | 142,135 | 5,048 | 3,212 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 33.46 | 20.46 | 10.46 | 18.24 | 16.43 | 0.58 | 0.37 |

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha sifa ya uoto wa savana.  Ni asilimia 20.46 tu ya watahiniwa waliweza kujibu swali kwa usahihi kwa kuchagua B “Nyasi ndefu”. Watahiniwa hawa waliweza kubaini kuwa nyasi ndefu hupatikana katika hali ya hewa ya Savana.  Asilimia 33.46 ya watahiniwa walichagua  A “Misitu minene” na asilimia 18.24 ya watahiniwa walichagua D “ Miti yenye umbile la mwamvuli” ambazo ni sifa ya hali ya hewa ya Ikweta. Chaguo C “Miti iliyochongoka juu” ni sifa ya uoto unaopatikana katika hali ya hewa ya baridi na chaguo E “Nyasi fupi” ni sifa ya uoto unaopatikana katika hali ya hewa ya kitropiki hivyo watahiniwa waliochagua majibu hayo hawakuwa na uelewa wa swali.

**Swali la 40:** Athari kuu za viwanda katika mazingira ni

A. Kuchafua maji, hewa na harufu mbaya
B. Kutoa moshi na matumizi makubwa ya nguvu ya nishati
C. Uchafuzi wa hewa, udongo na harufu mbaya
D. Kumwaga kemikali na kutoa moshi
E. Uchafuzi wa hewa, maji na ardhi.

Majibu ya Watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 245,774 | 135,313 | 91,652 | 133,659 | 251,309 | 3,960 | 3,502 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 28.41 | 15.64 | 10.59 | 15.45 | 29.05 | 0.46 | 0.40 |

Swali lilikuwa linapima uelewa wa watahiniwa kuhusu athari kuu za viwanda katika mazingira. Jibu sahihi lilikuwa ni E "Uchafuzi wa hewa, maji na ardhi". Ni asilimia 29.05 tu ya watahiniwa waliweza kulijibu swali hili kwa usahihi. Majibu mengine ya watahiniwa yalikuwa na mgawanyiko unaoonesha kuwa watahiniwa walikuwa na uelewa mdogo wa athari kuu za viwanda katika mazingira. Asilimia 28.41 ya watahiniwa waliochagua A "Kuchafua maji, hewa na harufu mbaya" na asilimia 10.59 walichagua C "Uchafuzi wa hewa, udogo na harufu mbaya", walishindwa kubaini kuwa harufu mbaya inatokana na uchafuzi wa hewa. Asilimia 15.64 ya watahiniwa waliochagua B "Kutoa moshi na matumizi makubwa ya nguvu ya nishati" hawakuwa na uelewa wa jibu. Watahiniwa asilimia 15.45 waliochagua D walikuwa na ufahamu kuhusu athari ndogondogo za viwanda katika mazingira lakini walishindwa kubaini athari kuu za viwanda kama ilivyoainishwa katika kiini cha swali.

**Swali la 41:** Zao la mkonge hulimwa katika mikoa ipi Tanzania?

A. Tanga na Mbeya.
B. Morogoro na Pwani.
C. Morogoro na Tanga.
D. Kilimanjaro na Manyara.
E. Mtwara na Singida.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 221,001 | 139,216 | 271,703 | 116,091 | 109,130 | 4,886 | 3,142 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 25.54 | 16.09 | 31.40 | 13.42 | 12.61 | 0.56 | 0.36 |

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha mikoa ya Tanzania ambayo zao la Mkonge hulimwa. Mtawanyiko wa ufaulu wa watahiniwa katika swali hili unathihirisha uelewa mdogo walionao watahiniwa juu ya kilimo cha zao la Mkonge katika nchi ya Tanzania. Ni asilimia 31.40 tu ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni C "Morogoro na Tanga". Asilimia 25.54 ya watahiniwa walichagua A "Tanga na Mbeya" hali inayoonesha

kuwa watahiniwa wengi hawajui mgawanyo wa mazao na mikoa inayolima mazao hayo. Watahiniwa waliochagua chaguo B (16.09%), D (13.42%) na E (12.61%) hawakuwa na uelewa wa jibu sahihi.

**Swali la 42:** Mambo muhimu katika ramani ni

A. Uoto, dira, kipimio, mistari na jina la ramani
B. Rangi, jina la ramani, kipimio, ufunguo na fremu
C. Mistari, jina la ramani, dira, fremu na kipimio
D. Jina la ramani, ufunguo, fremu, kipimio na dira
E. Jina la ramani, ufunguo, kipimio, dira na mistari.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 98,161 | 137,147 | 105,379 | 378,485 | 138,701 | 4,086 | 3,210 |
| Asilimia ya watahiniwa | 11.35 | 15.85 | 12.18 | 43.75 | 16.03 | 0.47 | 0.37 |

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha mambo muhimu yanayotakiwa kuwepo katika ramani. Mambo haya husaidia kurahisisha usomaji wa ramani. Asilimia 43.75 ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni D “Jina la ramani, ufunguo, fremu, kipimio na dira”. Aidha, majibu ya watahiniwa wengine yalitawanyika, ambapo asilimia 12.18 ya watahiniwa walichagua C “Mistari, jina la ramani, dira, fremu na kipimio” na asilimia 16.3 ya watahiniwa walichagua E “Jina la ramani, ufunguo, kipimio, dira na mistari”. Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa mistari siyo kitu muhimu katika ramani. Watahiniwa waliochagua chaguo A (11.35%) na B (15.85%) nao walishindwa kubaini kuwa rangi na uoto ni vipotoshi ambavyo katika ramani vinaelezewa katika ufunguo.

**Swali la 43:** Ipi kati ya zifuatazo ni njia ya kuzuia mafuriko?

A. Kujenga nyumba imara.
B. Kupanda miti.
C. Kukata miti.
D. Kuchoma misitu.
E. Kujenga nyumba mabondeni.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 174,999 | 466,926 | 76,749 | 52,609 | 86,083 | 4,915 | 2,888 |
| Asilimia ya watahiniwa | 20.23 | 53.97 | 8.87 | 6.08 | 9.95 | 0.57 | 0.33 |

Swali hili lilitahini uelewa wa watahiniwa kuhusu njia za kuzuia mafuriko. Swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwani watahiniwa wengi 53.97% waliweza kuchagua jibu sahihi B ‘Kupanda miti’. Watahiniwa waliochagua C (8.87%), D (6.08%) na E (9.95%) walishindwa kubaini kuwa sababu zilizoainishwa katika vipotoshi hivyo zinachochea kuwepo kwa mafuriko. Chaguo A “Kujenga nyumba imara” liliwavutia asilimia 20.23 ya watahiniwa kwani waliamini kuwa nyumba imara haziwezi kubomoka mafuriko yakitokea. Watahiniwa hawa walishindwa kubaini kuwa wanatakiwa kupanda miti ili kuzuia kasi ya mafuriko ambayo yanaweza kusababisha uharibifu katika sehemu ya makazi au katika mashamba.

**Swali la 44:** Sehemu ya jangwa ambayo maji hupatikana huitwa

A. Chemchemi
B. Visiwa
C. Oasis
D. Mito
E. Bonde.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 286,169 | 120,736 | 277,970 | 105,653 | 67,764 | 3,747 | 3,130 |
| Asilimia ya watahiniwa | 33.08 | 13.96 | 32.13 | 12.21 | 7.83 | 0.43 | 0.36 |

Swali lilipima uwezo wa watahiniwa kutambua sehemu ya jangwa ambayo maji hupatikana. Asilimia 32.13 ya watahiniwa walibaini jibu sahihi ambalo ni C “Oasis”. Watahiniwa hawa walifahamu kuwa Oasis ni sehemu inayopatikana maji katika jangwa ambayo hutokea baada ya mmomonyoko wa udongo unaosababishwa na upepo kuufikia mwamba wenye maji. Aidha, asilimia 33.08 ya watahiniwa waliochagua A “Chemchemi”, asilimia 12.21 waliochagua D “Mito” na asilimia 7.83 waliochagua E “Bonde”, walikuwa na uelewa wa jumla wa sehemu mbalimbali zinazopatikana maji lakini walishindwa kuelewa kuwa Oasis ni sehemu pekee kati ya vipotoshi vilivyotolewa katika swali hili ambayo maji hupatikana katika jangwa kwani chemchemi, mito na mabonde hupatikana katika maeneo mengine ya hali ya hewa. Aidha, asilimia 13.96 ya watahiniwa waliochagua B “Visiwa” walikuwa na uelewa kuwa visiwa vimezungukwa na maji, lakini wakashindwa kuelewa kuwa katika hali ya jangwa hakuna visiwa.

**Swali la 45:** Faida ya matumizi mrudio katika utunzaji wa mazingira ni

A. Kupanga kazi mradi
B. Uzalishaji wa bidhaa mbalimbali
C. Kupunguza taka
D. Kutengeneza taka
E. Kuuza taka.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 92,782 | 360,988 | 292,118 | 64,281 | 47,303 | 5,109 | 2,588 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 10.72 | 41.72 | 33.76 | 7.43 | 5.47 | 0.59 | 0.30 |

Swali lilitahini uelewa wa watahiniwa kuhusu faida za matumizi mrudio katika utunzaji wa mazingira. Asilimia 33.76 ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi C 'Kupunguza taka'. Asilimia 41.72 ya watahiniwa waliandika chaguo B 'Uzalishaji wa bidhaa mbalimbali', walishindwa kutambua kuwa hiyo ni faida ya matumizi mrudio kiuchumi wakati swali lilihusu faida ya matumizi mrudio katika utunzaji wa mazingira. Aidha, watahiniwa waliochagua A (10.72%), D (7.43%) na E (5.47%) hawakuwa na uhakika wa jibu sahihi na asilimia 0.59 ya watahiniwa hawakujibu swali hili.

**Swali la 46:** Jua linaonekana kubwa kuliko nyota zingine kwa sababu

A. Lina joto kali kuliko nyota zingine
B. Lina mwanga mkali kuliko wa nyota zingine
C. Linatupatia nguvu ya jua
D. Liko mbali sana na dunia
E. Liko karibu zaidi na dunia.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 112,679 | 280,762 | 74,715 | 125,329 | 263,419 | 4,480 | 3,785 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 13.02 | 32.45 | 8.64 | 14.49 | 30.45 | 0.52 | 0.44 |

Swali lilitahini uelewa wa watahiniwa kuhusu sababu zinazolifanya jua kuonekana kubwa kuliko nyota zingine. Ni asilimia 30.45 tu ya watahiniwa waliweza kutambua jibu sahihi kwa kuchagua E "Liko karibu zaidi na dunia". Watahiniwa 280,762 ambao ni sawa na asilimia 32.45 walichagua B "lina mwanga mkali kuliko wa nyota zingine", Asilimia 13.02 walichagua A "Lina

joto kali kuliko nyota zingine" na asilimia 14.47 walichagua D "Liko mbali sana na dunia". Watahiniwa hao hawakutambua matakwa ya swali. Aidha, asilimia 8.64 ya watahiniwa waliochagua C "Linatupatia nguvu ya jua" walishindwa kuelewa kuwa swali lilitaka sababu ya jua kuonekana kubwa kuliko nyota nyingine na siyo faida ya jua.

**Swali la 47:** Shirika la umoja wa mataifa linalohusika na uthibitisho wa ubora wa mazao huitwa

A. UNICEF
B. FAO
C. WHO
D. UNESCO
E. UNHCR.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 108,269 | 434,698 | 126,540 | 113,992 | 74,542 | 4,079 | 3,049 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 12.51 | 50.24 | 14.63 | 13.18 | 8.62 | 0.47 | 0.35 |

Swali hili lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kubaini shirika la Umoja wa Mataifa linalohusika na uthibitisho wa ubora wa mazao. Watahiniwa wengi walikuwa na uelewa wa swali hili kwani zaidi ya nusu ya watahiniwa (50.24%) walijibu kwa usahihi kwa kuandika B "FAO". Hata hivyo watahiniwa waliochagua A (12.51%), C (14.63%), D (13.18%) na E (8.62%) walishindwa kuelewa kuwa UNICEF ni shirika linaloshughulikia watoto, WHO linashughulikia afya, UNESCO linahusika na elimu, sayansi na utamaduni na UNHCR linashughulikia wakimbizi. Aidha asilimia 0.47 ya watahiniwa hawakujibu swali hili.

**Swali la 48:** Maeneo ambayo ufugaji wa jadi hufanyika kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania ni

A. Lindi, Mtwara, Shinyanga, Mwanza na Mbeya
B. Kigoma, Mwanza, Kilimanjaro, Arusha na Lindi
C. Shinyanga, Mwanza, Dodoma, Arusha na Mara
D. Mwanza, Shinyanga, Mbeya, Tanga na Morogoro
E. Mwanza, Shinyanga, Mbeya, Tanga na Lindi.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 130,081 | 165,592 | 309,279 | 160,098 | 92,240 | 4,743 | 3,136 |
| Asilimia ya watahiniwa | 15.04 | 19.14 | 35.75 | 18.50 | 10.66 | 0.55 | 0.36 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua maeneo ambayo ufugaji wa jadi hufanyika kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania. Jibu sahihi la swali hili ni C "Shinyanga, Mwanza, Dodoma, Arusha na Mara" ambalo lilichaguliwa na asilimia 35.75 ya watahiniwa. Hii inaashiria kuwa watahiniwa wengi wanafahamu mikoa maarufu katika ufugaji wa jadi. Watahiniwa waliochagua vipotoshi A (15.04%), B (19.14%), D (18.50%) na E (10.66%) walishindwa kutambua kuwa katika mikoa ya Lindi, Tanga, Mbeya na Mtwara ufugaji wa jadi haufanyiki kwa kiwango kikubwa. Hata hivyo swali hili halikujibiwa na watahiniwa 4,743 ambao ni sawa na asilimia 0.55 ya watahiniwa waliofanya mtihani.

**Swali la 49:** Mgawanyo wa Bonde la Ufa la Afrika Mashariki na kuunda tawi la Mashariki na Magharibi umeanzia ziwa

A. Viktoria
B. Tanganyika
C. Natroni
D. Nyasa
E. Manyara.


Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 281,764 | 221,238 | 130,762 | 171,604 | 53,495 | 3,853 | 2,453 |
| Asilimia ya watahiniwa | 32.57 | 25.57 | 15.11 | 19.83 | 6.18 | 0.45 | 0.28 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua Ziwa ambalo mgawanyo wa Bonde la Ufa la Afrika Mashariki ulipoanzia na kuunda tawi la mashariki na magharibi. Jibu sahihi ni D 'Nyasa' ambalo lilichaguliwa na asilimia 19.83 tu ya watahiniwa. Asilimia 32.57 ya watahiniwa walichagua A 'Victoria'. Mwelekeo huu wa majibu unadhihirisha kuwa watahiniwa hawafahamu ramani ya Afrika Mashariki na mgawanyo wa Bonde la Ufa la Afrika Mashariki kwani ziwa Victoria haliko katika Bonde la Ufa. Asilimia 25.57 ya watahiniwa waliochagua B 'Tanganyika" wanafahamu kuwa ziwa Tanganyika lipo katika bonde la ufa la Afrika Mashariki lakini walishindwa

kutambua kuwa halipo katika mwanzo wa mgawanyo wa bonde hilo. Aidha watahiniwa waliochagua C (15.11%) na E (6.18%) walishindwa kufahamu jibu sahihi na watahiniwa 3,853 (0.45%) hawakujibu kabisa swali hili.

**Swali la 50:** Soma ramani ya mistari ya kontua kisha jibu swali linalofuata:




Herufi **' b '** inawakilisha umbo gani la sura ya nchi?

A. Genge.
B. Bonde.
C. Mwinuko.
D. Kigongo.
E. Kilima.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Hawakujibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 115,100 | 324,497 | 179,645 | 153,211 | 87,446 | 2,867 | 2,403 |
| Asilimia ya watahiniwa | 13.30 | 37.51 | 20.76 | 17.71 | 10.11 | 0.33 | 0.28 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kusoma ramani ya kontua na kutambua umbo la sura ya nchi lililowakilishwa na herufi 'b'. Watahiniwa wengi hawakuwa na uelewa wa swali hili. Jibu sahihi ni D 'Kigongo' ambalo lilichaguliwa na asilimia 17.71 tu ya watahiniwa. Asilimia kubwa ya watahiniwa (37.51%) walichagua B 'Bonde'. Mwelekeo huu wa majibu unadhihirisha kuwa watahiniwa hawafahamu tofauti iliyopo kati ya bonde na kigongo katika ramani ya kontua. Watahiniwa wengi wameshindwa kufahamu kuwa

katika ramani ya kontua, kigongo huwakilishwa na mistari ya kontua yenye umbo la V au U iliyoangalia juu ya mlima na bonde huwakilishwa na mistari ya kontuo yenye umbo la V au U iliyoangalia chini ya mlima. Watahiniwa waliochagua A (13.30%), C (20.76%) na E (10.11) hawakujua jibu sahihi. Aidha, watahiniwa 2,867 (0.33%) hawakujibu swali hili.

## 3.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa wengi hawakuwa na uelewa katika baadhi ya maswali jambo linalooneshа kuwa watahiniwa hawakuwa na ujuzi wa kutosha katika baadhi ya mada. Hali hii imebainika katika baadhi ya mada kwani katika maswali ambayo chaguzi zake hazikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na maswali yaliyoulizwa, baadhi ya watahiniwa waliyachagua. Baadhi ya mada ambazo watahiniwa wameonekana kutokuwa na uelewa wa kutosha ni Uongozi Katika Familia, Serikali za Mitaa na Vijiji, Serikali Kuu; Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tanzania Huru, Afrika Huru, Uvamizi wa Kimataifa, Mahusiano ya Watanzania na Jamii za Kigeni, Stadi za Ramani, Hali ya Hewa na Mazingira.

## 4.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha elimu na ufaulu kwa ujumla tunashauri yafuatayo:

(a) Wanafunzi wasome vitabu vya kiada na ziada ili kuboresha uelewa wao katika mada mbalimbali.

(b) Kuweka mkazo zaidi katika ufundishaji wa mada ambazo ufaulu wake haukuwa mzuri katika mtihani huu.

(c) Walimu wafundishe mada zote kwa ukamilifu.

(d) Katika mitihani ya mihula na mazoezi ya darasani walimu watunge maswali yanayoweza kupima na kujenga uwezo wa wanafunzi kujibu maswali yanayohitaji kufikiri ili waweze kufanya vizuri katika mtihani wa Taifa.